# KUTAYARISHA FAMILIA YAKO

## KWA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA UHAMIAJI

Jua Haki Zako

Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

immigration.ablelaw.org

# YALIYOMO

**KABLA YA KUSHAMBULIWA GHAFLA KWA SABABU ZA UHAMIAJI........................................................................ 2**
UNDA MPANGO WA DHARURA JINSI UTAKAVYOSHUGHULIKIA SHAMBULIZI HILO ILI ULINDE FAMILIA YAKO!

**JUA HAKI ZAKO.......................................................................... 3**
CHA KUFANYA UNAPOKUTANA NA POLISI AU MAOFISA WA UHAMIAJI

**TAARIFA KUHUSU WANAOZUILIA WATU KWA SABABU YA UHAMIAJI..............................................................................6**

**IKIWA UMEZUILIWA KWA SABABU YA UHAMIAJI......... 7**

**KIAMBATISHO CHA A....................................................... 8**
WANAOTOA HUDUMA ZA KISHERIA ZA UHAMIAJI BILA LENGO LA FAIDA

**KIAMBATISHO CHA B..................................................... 10**
FOMU & TAARIFA MUHIMU YA KIBINAFSI

Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi..........................................................................................11

Nambari Muhimu za Simu & Taarifa Muhimu ...............................................................13

Rekodi Muhimu za Familia..................................................................................................14

Taarifa ya Familia ya Matibabu & Utambulisho .............................................................15

Watu wa Kuwasiliana nao ukiwa na Shida za Kisheria, Wizi wa Utambulisho, & Udanganyifu.......................................................................................................................17

Huduma ya Dharura ya wanyama vipenzi..........................................................................18

**KIAMBATISHO CHA C..................................................... 19**
NAMBARI MUHIMU

Taarifa kwa Wahamiaji Waliozuiliwa & Mawakili wa Wahamiaji katika jimbo la Ohio................................................................................................................... 19

Mfumo wa ICE wa Mtandaoni wa Kutafuta Waliozuiliwa............................................ 19

Ofisi za Serikali.................................................................................................................. 19

Vituo vya Kuzuilia Watu.................................................................................................... 21

Vituo vya Kuzuilia Watu katika Jimbo la Ohio.............................................................. 22

Orodha ya Ubalozi Mdogo/Ubalozi................................................................................. 23

Kusajili Watoto Wako Waliozaliwa Marekani katika Nchi ya Nyumbani....................... 24

Baadhi ya taarifa na fomu zilizotumiwa katika chapisho hili ni kwa hisani ya Kituo cha Haki za Wahamiaji cha Michigan (Michigan Immigrant Rights Center).

# KABLA YA KUSHAMBULIWA GHAFLA KWA SABABU ZA UHAMIAJI

UNDA MPANGO WA DHARURA JINSI UTAKAVYOSHUGHULIKIA SHAMBULIZI HILO ILI ULINDE FAMILIA YAKO!

## Weka hati zako zote muhimu pahali ambapo utazipata kwa urahisi.

Chapisha nakala zingine za hati zako na umpatie mwanafamilia au rafiki wa karibu akuwekee kwa ajili ya nyakati za dharura.

- Pasipoti
- Cheti cha Kuzaliwa
- Leseni ya Ndoa
- Hati za Mali
- Hati zote za uhamiaji, ikiwa ni pamoja na nambari ya "Mha

## Zungumza na wakili wa uhamiaji asiyepata faida ili achunguze hali yako binafsi ya uhamiaji.

- Hakikisha kwamba una nambari au kadi ya mtoa huduma ya kisheria au wakili wa uhamiaji anayeheshimika endapo dharura itokee. Angalia KIAMBATISHO CHA A ili uone orodha.
- Wanafamilia wako wengine pia wanafaa kuwa na nambari hizi.

## Hakikisha kwamba una mpango kazini mwako unaoelezea jinsi utakavyoshughulikia hali ya dharura.

- Maofisa wa uhamiaji wakija kazini mwako, waulize wafanyakazi wenzako kama wanaweza kuwa kimya; omba uzungumze na wakili.
- Ikiwa kuna muungano wa wafanyakazi kazini mwako, zungumza na mwakilishi wa muungano ili ujifunze vizuri jinsi ya kujitayarisha ili upambane na shambulizi.

## Kuwa na mpango wa kulinda familia yako.

- Tayarisha fomu ya "Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi" ndio uhakikishe kwamba watoto wako watatunzwa na jamaa au rafiki wa familia endapo umezuiliwa.
    - » Hii ni muhimu sana, na katika hali ya dharura, itamruhusu rafiki wa karibu au mwanafamilia awalinde watoto wako badala ya wao kuwekwa waishi na watu wengine wasiowajua kwenye mfumo wa ulezi wa kambo. Angalia KIAMBATISHO CHA B ili uone orodha.
- Chukua pasipoti halali kwa ajili ya watoto wako.
    - » Ikiwa mtoto wako ni raia wa Marekani, mchukulie pasipoti haraka iwezekanavyo. Watahitaji pasipoti ili wasafiri nje ya nchi.
    - » Ikiwa mtoto wako si raia wa Marekani, mchukulie pasipoti kutoka nchi aliyozaliwa. Unaweza kupata pasipoti hii kutoka kwa ubalozi mdogo wa nchi yako. Angalia KIAMBATISHO CHA C ili uone orodha.
- Sajili mtoto wako kama raia wa nchi yako ya nyumbani katika ubalozi mdogo wa nchi hiyo ili usiwe na shida katika nchi hiyo utakapowasili huko.
    - » Kwa mfano, katika nchi zingine, watoto ambao hawajasajiliwa hawawezi kuenda shule. Angalia ukurasa wa 24 kwa taarifa kuhusu jinsi ya kusajili watoto wako waliozaliwa Marekani katika nchi ya nyumbani.

# JUA HAKI ZAKO

## UNACHOFAA KUFANYA UKIKUTANA NA POLISI AU MAOFISA WA UHAMIAJI

### Mambo Maalum ambayo Wasio-raia (Wageni) Wanafaa Kuzingatia:

- Unahitaji kujitayarisha endapo utakamatwa. Panga mipango na familia yako. Kariri nambari za simu za watu muhimu wa kuwasiliana nao, ikiwa ni pamoja na wakili wako.
- Usizungumzie hali yako ya uhamiaji na mtu mwingine yeyote isipokuwa wakili wako.
- Muulize wakili wako kuhusu kitakachotendeka iwapo umefungwa jela au endapo maelezo ya kushtakiwa kwako yamefikishwa mahakamani kwa sababu ya hali yako ya uhamiaji. Ikiwa uko kwenye jela, huenda ofisa wa uhamiaji akakutembelea. Usijibu maswali yoyote au kutia saini chochote kabla ya kuzungumza na wakili wako.
- Soma karatasi zote kwa makini. Mwambie ofisa huyo au ajenti huyo ikiwa unahitaji mkalimani/mtafsiri.

### Haki Zako:

- Una haki ya kutojibu maswali. Ikiwa ungependa kutekeleza haki hii, sema hivyo kwa sauti inayosikika kisha unyamaze. **Kumbuka kwamba chochote unachosema kinaweza kutumiwa dhidi yako.**
- Hata hivyo, katika jimbo la Ohio, kuna jambo la kipekee kuhusu haki yako ya kunyamaza. Ikiwa polisi wanashuku ya kutosha kwamba umetenda uhalifu, au unapanga kutenda uhalifu, lazima useme jina lako, anwani yako, na tarehe yako ya kuzaliwa. Baada ya kumpatia ofisa wa polisi taarifa hii hauhitajiki kujibu maswali mengine yoyote.
- Una haki ya kukataa upekuzi ufanywe kwako wewe mwenyewe, kwenye gari lako, au nyumbani mwako.
- Una haki ya kushughulikiwa kwa heshima na polisi.
- Ikiwa haujakamatwa, una haki ya kuondoka polepole kwa utulivu.
- Ikiwa umekamatwa na kushtwakiwa kwa uhalifu, una haki ya kumuona wakili. Itisha wakili haraka.
- Bila kujali hali yako ya uhamiaji au ya uraia, una haki za kikatiba.

### Majukumu Yako:

- Kuwa mtulivu na mpole.
- Usivuruge wala kuzuia shughuli za polisi. Fuata maagizo yote ya kimwili ya ofisa huyo.
- Usikatae shughuli za ofisa kwa kutumia mwili wako, hata kama unaamini kwamba hawakutendei haki.
- Usidanganye wala usionyeshe hati bandia.
- Kumbuka maelezo kuhusu tukio hilo na uyaandike haraka iwezekanavyo.

## Ikiwa Umesimamishwa Wakati Unaendesha Gari

- Simamisha gari hilo pahali salama haraka iwezekanavyo. Weka mikono yako kwenye steering ya kuendeshea gari na usifanye chochote kingine hadi ofisa afike kwenye dirisha lako.
- Usiondoke kwenye gari, usijaribu kutoroka, au usifanye chochote cha kighafla.
- Ukiombwa, onyesha polisi leseni yako ya dereva, usajili, na uthibitishe kwamba una bima.
- Ofisa au ajenti wa uhamiaji akiomba aangalie kwenye gari lako, unaweza kukataa asifanye utafutaji kwenye gari lako. Ili haki zako zingine zidumishwe, lazima useme kwa uwazi kwamba unakataa wafanye utafutaji.
- Polisi wanaweza “kugusa” nguo zako ikiwa wanashuku kwamba una silaha ambayo imefichwa. Hufai kukataa au kupambana nao, hata hivyo lazima useme kwa uwazi kwamba umewanyima ruhusa ya kufanya utafutaji.
- Madereva na abiria wana haki ya kukataa kuzungumza. Ikiwa wewe ni abiria, unaweza kuwauliza ikiwa unaweza kuondoka. Ofisa akisema ndiyo, kaa kwa utulivu au uondoke kwa upole. Hata kama ofisa amesema hapana, una haki ya kukataa kuzungumza.
- Usikatae kukamatwa, hata kama unaamini kwamba huna hatia.
- Ukipewa tiketi, tia saini kwenye tiketi hiyo; usipoitilia saini, unaweza kukamatwa. Bado unaweza kupeleka kesi hiyo mahakamani baadaye.

## Ukiulizwa Maswali Kuhusu Hali Yako ya Uhamiaji

- Kumbuka kwamba una haki ya kukataa kuzungumza. Huhitajiki kuzungumzia hali yako ya uhamiaji au uraia na polisi, maajenti wa uhamiaji, au maafisa wengine wowote. Huhitaji kujibu maswali kuhusu ulizaliwa wapi, iwapo wewe ni raia wa Marekani, ama jinsi ambavyo uliingia nchini.

- Sheria ya kitaifa inahitaji kwamba wasio-raia (wageni) wabebe hati zao halali za uhamiaji kila wakati. Ajenti wa uhamiaji (Ofisa wa Mipaka au Maofisa wa Uhamiaji na Forodha (“ICE”)) akiukuomba karatasi zako za uhamiaji ili aziangalie, utakuwa unavunja sheria ya kitaifa usipopeana karatasi hizi halali za uhamiaji ikiwa unazo.

Usidanganye kuhusu hali yako ya uraia wala usipeane hati bandia. Andika kila kitu unachokumbuka, ikiwa ni pamoja na nambari ya beji ya ofisa na nambari ya magari ya polisi ya kupiga doria, shirika ambalo maofisa hao wanatokea, na maelezo yoyote mengine.

KUMBUKA

**Una haki ya kukataa kuzungumza.**
**Usiseme chochote kuhusu hali yako ya uhamiaji au pahali ambapo ulizaliwa. Ikiwa unakaratasi halali za uhamiaji, zionyeshe.**

## Maofisa wa Polisi au wa Uhamiaji Wakija Nyumbani Mwako


Maofisa wa polisi au wa uhamiaji wakija nyumbani mwako, **USIFUNGUE MLANGO**. Una haki ya kuwakataza wasiingie isipokuwa kama wana vibali au hati fulani. Muombe afisa au ajenti huyo aingize hati/kibali hicho kupitia chini ya mlango au aibebe karibu na dirisha ili uweze kukisoma/kukikagua.

- Kibali cha utafutaji huwapatia polisi haki ya kuingia kwenye nyumba/eneo lililoandikwa kwenye kibali hicho, hata bila ruhusa yako, lakini maofisa wanaweza kufanya utafutaji kwenye maeneo na vitu vilivyoandikwa kwenye hati/kibali hicho pekee. Kibali cha utafutaji lazima kitiwe saini na jaji. Omba upewe risiti ya chochote ambacho ofisa huyo amekitoa nje ya nyumba yako.
- Kibali cha kumkamata mhalifu huwaruhusu mapolisi kuingia kwenye nyumba ya aliyetajwa kwenye kibali hicho kama wanaamini kwamba mtu huyo yuko ndani ya nyumba hiyo. Kibali cha kumkamata mhalifu lazima kitiwe saini na jaji.
- Kibali cha kumuondoa/kumfukuza mtu nchini ("Kibali cha ICE") HAKIRUHUSU maofisa kuingia nyumbani bila ruhusa.

Hata kama maofisa wako na hati/kibali, una haki ya kukataa kuzungumza. Ukiamua kuongea na maofisa hao, toka nje na ufunge mlango. Hata hivyo, inkatik ahali zingine za dharura, maofisa wa polisi wanaweza kuingia nyumbani mwako na kufanya utafutaji/upekuzi bila kibali (kwa mfano, wakati mtu amepiga mayowe kwamba asaidiwe akiwa ndani ya nyumba hiyo au wakati mapolisi wanamfuata mtu ili wamshike).

## Ukikamatwa

- Omba uzungumze na wakili wako au omba upige simu.
- Wasiliana na rafiki yako unayemwamini au mwanafamilia anayejua nambari ya wakili wako na anayejua utakachofanya wakati wa dharura. Kariri nambari za simu za utakayewasiliana naye.
- Wasiliana na ubalozi wako mdogo. Una haki ya kumwambia ajenti ajulishe ubalozi mdogo wako kuhusu kukamatwa kwako. Ubalozi wako unaweza kukusaidia kupata wakili ikiwa huna wakili na pia unaweza kuwasiliana na familia yako.



**Usitie saini kwenye chochote ambacho hauelewi kabla hujapata ushauri wa wakili wako!**

Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

# TAARIFA KUHUSUWANAOZUILIA WATU KWA SABABU YA UHAMIAJI

**Je, serikali ya ndani inaweza kumzuilia mtu kwa muda gani wakiombwa na ICE wamzuilie mtu?**

Kulingana na sheria za kitaifa, mtu ambaye amezuiliwa na mzuiaji wa uhamiaji hawezi kuzuiliwa kwa zaidi ya saa 48, bila kujumuisha siku za Jumamosi, Jumapili, na siku za likizo. Kipindi hiki cha saa 48 huanza baada ya mapolisi wa ndani au jimbo wameshamwachilia mtu huyo kwa sababu ya hatia yoyote. Mzuiaji anaweza kuulizwa maswali iwapo amekuzuia bila sababu.




**Je, nini hutendeka baada ya saa 48 kuisha?**

Kwa vile uzuiaji wa ICE huruhusu mtu azuiliwe kwa saa 48 baada ya muda unaoruhusiwa na sheria ya ndani au ya jimbo kuisha, ikiwa mzuiaji huyo ana sababu ya kumzuilia mtu huyo, mtu huyu aliyezuiliwa anapaswa kuachiliwa haraka baada ya kipindi cha saa 48 kuisha. Baada ya kipindi hiki, wewe na/au wakili wako mnapswa kuomba kwamba uachiliwe iwapo haujaachiliwa kiotomatiki.



**Je, nini hutendeka iwapo jela imeendelea kumzuilia mtu wakati muda wa amri umekwisha?**

Ikiwa jela hiyo haina mamlaka ya kipekee ya kumzuia mtu kwa sababu za mashtaka ya uhalifu, ni hatia kwao kuendelea kumzuilia mtu huyo baada ya kipindi cha kumzuia mtu kwa sababu za uhamiaji kuisha. Wasiliana na wakili kama hili limetendeka.



## DHAMANA

Saa 48 huanza baada ya mtu kulipa dhamana ya shtaka la uhalifu, au vinginevyo huanza kama ameachiliwa na polisi. Kuna uwezekano kwamba ICE inaweza kumchukua mtu huyo akishalipa dhamana ya ndani/jimbo, na kwamba muda ambao mtu amezuiliwa kwa uhamiaji hautaongezwa kwenye muda wa kifungo. Ikiwezekana, pata ushauri wa wakil haraka iwezekanavyo baada ya kuzuiliwa ili uone kama kulipa dhamana ya ndani ni jambo la busara. **Usitegemee ushauri kutoka kwa karani au wafanyakazi wa jela kuhusu suala hili.**

# IKIWA UMEZUILIWA KWA SABABU YA UHAMIAJI

## Wakati ambapo upo kwenye kituo cha kuzuiliwa kwa sababu za uhamiaji, una haki ya:

- Kushughulikiwa kwa heshima
- Kupokea kitabu cha mtu aliye kizuizini
- Kupata vifaa vya kisheria na kumpata wakili utakayemlipa wewe mwenyewe
- Kupiga simu
- Kutembelewa
- Kuwasiliana na ubalozi wako
- Kutotia saini kwenye hati au kauli ambazo huelewi
- Mawasiliano ya barua au ya kimaandishi
- Burudani
- Kuabudu
- Pesa na mali yako binafsi
- Matibabu

## Ikiwa Umefikishwa Mahakamani kwa Kesi ya Kuondolewa (Kufukuzwa) Nchini

- Una haki ya kumwajiri wakili, lakini serikali haitakupatia wakili katika Mahakama ya Uhamiaji. Ikiwa huna wakili, omba orodha ya wakili wasiolipwa au wanaotoza pesa kidogo.
- Kumbuka kwamba una haki ya kunyamaza kimya. Chochote ambacho umesema kinaweza kutumiwa dhidi yako baadaye.
- USITIE saini kwenye chochote ambacho huelewi kabla ya kuongea na waklili wako kwanza. Mwambie ajenti ikiwa unahitaji mkalimani/mtafsiri au ikiwa unahitaji hati fulani itafsiriwe.
- Kumbuka nambari yako ya mgeni ("Nambari") ana upatie wanafamilia wako nambari hii. Nambari hii itsaidia wanafamilia kukutafuta.
- Weka hati zote ambazo umepewa pahali salama.

## Haki katika Mahakama ya Uhamiaji

Ikiwa Umefikishwa Mahakamani kwa Kesi ya Kuondolewa (Kufukuzwa) Nchini, na hapo awali amri haikuwa imetolewa kwamba uondolewe nchini, una haki ya kuwasilisha kesi yako kwa jaji wa uhamiaji. Unaweza kuondoa haki yako ya kusikizwa mahakamani ikiwa umetia saini kwenye karatasi ukikubali kwamba uondolewe nchini bila kusikizwa mahakamani. Pia una haki ya:

- Kuwakilishwa na wakilii wakati kesi yako inasikizwa, lakini serikali haina wajibu/jukumu la kukupatia wakili.
- Kuomba dhamana.
- Kuwa na mkalimani wakati kesi yako inasikizwa ikiwa huzungumzi Kiingereza.

Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

# KIAMABATISHO CHA A:
## WANAOTOA HUDUMA ZA KISHERIA ZA UHAMIAJI BILA KUPATA FAIDA

### Orodha ya Wanaotoa Huduma za Kisheria za Uhamiaji bila kupata faida katika Jimbo la Ohio

Unashauriwa kwamba uzungumze na mashirika haya kabla ukuwe na shida na mamlaka ya uhamiaji ili uchunguze hali yako binafsi na uone ikiwa kuna mambo yanayoweza kukusaidia/kukuokoa endapo umezuiliwa.

**Mashirika ambayo huwa yanawakilisha watu katika kesi za kuondolewa nchini na masuala/mambo mengine ya uhamiaji:**

**Advocates for Basic Legal Equality, Inc.**

130 W. Second St., Ste. 700
Dayton, OH 45402

525 Jefferson Ave., Ste. 300
Toledo, OH 43604

(800) 837-0814

**immigration.ablelaw.org**

**Dayosisi ya Catholic Charities ya Cleveland**
*Huduma za Uhamiaji & Ukimbizi*
*Huduma za Kisheria za Uhamiaji*

7800 Detroit Ave.
Cleveland, OH 44102

(216) 939-3769

**ccdocle.org/program/immigration-legal-services**

**Catholic Charities Legal Immigration Services (Huduma za Kisheria za Uhamiaji za Catholic Charities**

206 W. Main St.
Ravenna, OH 44266

4200 Park Ave., 3rd Floor
Ashtabula, OH 44004

800 Market Ave. North, Ste. 1150
Canton, OH 44702

(330) 297-7250

**ccdoy.org/social-action/immigration-services**

**Catholic Charities Southwestern Ohio**

7162 Reading Rd., Ste. 700
Cincinnati, OH 45237

(513) 672-3746

**ccswoh.org**

**Centro San Jose El Trabajador**
**Immigrant Worker Project**

701 Walnut Ave. NE
Canton, OH 44702

(330) 454-2220

**iwpohio.org/english_version/program.htm**

**Community Refugee and Immigration Services**

1925 E. Dublin-Granville Rd., Ste. 102
Columbus, OH 43229

(614) 235-5747

**crisohio.org**

**International Institute of Akron**

207 E. Tallmadge Ave.
Akron, OH 44310

(330) 376-5106 ext. 102

**iiakron.org**

**International Institute of Greater Toledo**

3110 Tremainsville Rd.
Toledo, OH 43613

(419) 241-9178

**internationalinstituteoftoledo.org**

**Legal Aid Society of Cleveland**

1223 W. 6th St.
Cleveland, OH 44113

(216) 687-1900

**lasclev.org**

## Mashirika yanayowakilisha watu katika masuala/mambo mengine ya uhamiaji:

**Asian Services In Action, Inc. (ASIA)**

3631 Perkins Ave., Ste. 2A-W
Cleveland, OH 44114

(216) 881-0330 ext. 214

**asiaohio.org**

**Community Legal Aid**

11 Central Square, 7th Floor
Youngstown, OH 44503

(330) 983-2619

**communitylegalaid.org**

**Legal Aid Society of Southwest Ohio**

215 E. 9th St., Ste. 500
Cincinnati, OH 45202

10 Journal Square, Ste. 300
Hamilton, OH 45011

(513) 241-9400

**lasswo.org**

**Sisters of St. Francis**
**Project Hope / Proyecto Esperanza**

300 Short Buehrer Rd.
Archbold, OH 43502

(419) 445-0728

**tiffinfranciscans.org**

**St. Wendelin Parish – En Camino**

323 N. Wood St.
Fostoria, OH 44830

(419) 619-3625

**Vineyard Community Center**
*Immigration Counseling Services*

6000 Cooper Rd.
Westerville, OH 43081

(614) 259-5322

**vineyardcommunitycenter.org**

Kwa taarifa zaidi kuhusu mashirika haya na huduma
zao, tafadhali tembelea tovuti zao au

**immigrationadvocates.org/nonprofit/legaldirectory**

ili upate Orodha Kamili ya Kitaifa ya Huduma za Kisheria za Uhamiaji.



Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

# MAMLAKA KIDOGO YA UWAKILISHI

## MAAGIZO/MIELEKEZO

Mzazi au mlezi wa kisheria (Mhusika Mkuu) anapaswa kujaza fomu iliyoko kwenye kurasa za 11-12 ili ampatie asiyehusika moja kwa moja (Mwakilishi) mamlaka ya kawaida ya kufanya maamuzi na mambo mbalimbali ambayo mzazi humfanyia mtoto wake.

1. Unapaswa kuchapisha nakala za fomu hii baada ya kutiwa saini. Tumia nakala ulizochapisha ikiwezekana ili ulinde ile asilia.
2. Fomu hii inapaswa kutiwa saini na mzazi au wazazi ambao wana haki ya ulezi au mlezi wa kisheria. Wazazi wote wawili wanapaswa kutia saini ikiwa mtoto huyo anaishi na wazazi wote wawili.
3. Kila mtoto katika familia anapaswa kujaziwa fomu yake kivyake ya Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi.
4. Kutokana na matatizo ya usafiri ya kupeleka mtoto katika nchi nyingine, ni vizuri kwamba wazazi watie saini Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi inayomfanya mzazi huyo mwingine kuwa Mwakilishi, pamoja na Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi inayomfanya mwanafamilia mwingine au rafiki anayeaminika kuwa Mwakilishi.
5. Mzazi au wazazi lazima watie saini kwenye fomu hii mbele ya mthibitishaji rasmi. Ikiwa hukuwa umetia saini fomu ya Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi kabla ya kukamatwa au kuzuiliwa, unaweza kuwaomba wafanyakazi wa jela wakusaidie kupata mthibitishaji kwenye jela. Kila benki ina mthibitishaji rasmi. Huhitajiki kulipa pesa nyingi.
6. Fomu hii huenda isitimizwe au kutambuliwa na watu wote, mashirika yote ya serikali, au biashara zote.
7. Ukitia saini fomu ya Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi mapema, utahitaji kuitia saini tena ikiwa uliiwekea tarehe ya kukoma kutumika.
8. Fomu ya Mamlaka Kidogo ya Uwakilishi ni suluhisho ya muda mfupi tu wakati ambapo mzazi au wazazi wamekamatwa na kuzuiliwa na serikali. Mwakilishi atahitaji kushauriana na wakili kuhusu ulezi wa mtoto ikiwa mzazi wa mtoto au mlezi wa kisheria amezuiliwa.

# MAMLAKA KIDOGO YA UWAKILISHI KWA AJILI YA MTOTO NA MATIBABU, KUFIKIA REKODI ZA ELIMU, NA MAMLAKA YA KUFANYA MAAMUZI YA KIELIMU

**Mhusika Mkuu / Mzazi**

Jina: ______________________________

Tarehe ya Kuzaliwa:

Aina ya Kitambulisho:______________________

Nambari ya Kitambulishi:____________________

**Mhusika Mkuu / Mzazi**

Jina: ______________________________

Tarehe ya Kuzaliwa: ______________________

Aina ya Kitambulisho: ______________________

Nambari ya Kitambulishi: ____________________

**Mtoto**

Jina: ______________________________

Tarehe ya Kuzaliwa:______________________

SSN:______________________________

Nambari ya Pasipoti:______________________

**Mwakilishi**

Jina:______________________________

Tarehe ya Kuzaliwa:______________________

Anwani: ______________________________

______________________________

Mimi/Sisi, ______________________ na ______________________ , ambao kwa sasa tunaishi ______________________, kama wazazi/mzazi na/au mlezi/walezi wa ______________________, ambaye ametajwa hapa kama **mtoto**, tunapeana mamlaka kwa______________________ , ambaye ametajwa hapa kama **Mwakilishi** wangu/wetu, ya kutenda kwa niaba yetu katika masuala/majukumu yafuatayo kulingana na Kanuni Iliyosahihishwa ya Ohio Sura ya 1337 (Ohio Revised Code Chapter 1337):

1. Kuruhusu matibabu yoyote yanayohitajika, upasuaji, dawa, tiba, kuluazwa hospitalini au utunzaji au matibabu mengine kama haya kwa ajili ya mtoto;
2. Kuajiri, kuhifadhi au kufuta mtu yeyote ambaye anaweza kumtunza, kumshauri, kumtibu au kumsaidia mtoto kwa njia nyingine;
3. Kupokea Taarifa Inayolindwa ya Afya chini ya Sheria ya Kuhamisha Bima ya Afya na Uwajibikaji (HIPAA) kumhusu mtoto wangu/wetu, ikiwemo kupeana rekodi/taarifa;
4. Kupata nakala za rekodi za kielimu za mtoto wangu/wetu zilizowekwa kwenye faili za kielimu za mtoto wangu/wetu. Ni/Tunapeana idhini kwa taasisi za elimu ya kufichua au kupeana rekodi za elimu na kuwaondolea vikwazo walizowekewa na sheria, ikiwa ni pamoja na, bali sio tu, Sheria ya Haki za Kielimu za Familia na Faragha, 20 U.S.C. 1232g na Kanuni Iliyosahihishwa ya Ohio (Ohio Revised Code) Fungu la 3319.321;
5. Kuchangia maamuzi ya kielimu yanayohusu mtoto wangu/wetu kana kwamba Mwakilishi aliyetajwa hapa ni mzazi au mlezi wa mtoto. Ni/Tunawaondolea taasisi za elimu vikwazo walizowekewa na sheria za kuamua ni nani anayeweza kufanya maaumuzi ya kielimu kwa ajili ya mtoto wangu/wetu, ikiwa ni pamoja na, bali sio tu, Sheria ya Haki za Kielimu za Familia na Faragha, 20 U.S.C. 1232g na Kanuni Iliyosahihishwa ya Ohio (Ohio Revised Code) Fungu la 3319;
6. Kumpeleka mtoto wangu/wetu shuleni au kumchukua kutoka shuleni au kupeana ruhusa ya kuenda safari ya kielimu ya mtoto wangu/wetu. Ni/Tunawaondolea taasisi za elimu vikwazo walizowekewa na sheria za kuamua ni nani anaweza kumpeleka mtoto wangu/wetu shuleni au kumchukua kutoka shuleni au kupeana ruhusa ya kuenda safarini au kufanya shughuli za kielimu;

Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

7. Wawe na haki sawa za wazazi, ambazo mimi/sisi tunaweza kuwa nazo kuhusiana na utunzaji, ulezi na kuongoza mtoto na pia wawe na uhuru wa kutimiza haki hizi katika nyumba ya Mwakilishi wangu/wetu au pahali pengine ambapo Mwakilishi wangu/wetu amechagua yeye mwenyewe;
8. Kuidhinisha na kuruhusu kusafiri na mtoto kuenda na kutoka Marekani, na ndani ya ________________________________ na,
9. Kufanya vitendo vyote vingine vinavyohitajika, au vinavyohusika na utekelezaji wa masuala/mamlaka/majukumu yaliyotajwa hapa.

Pia ni/tunapendekeza na kuruhusu Mwakilishi wangu/wetu kuteuliwa na Mahakama ya Watoto kama mlezi wa kisheria endapo sitakuwepo/hatutakuwepo kwenye jimbo kwa siku 30 au zaidi.

Kitendo chohote cha kisheria ambacho kimetendwa na ajenti wangu/wetu kitatuwajibisha sisi wenyewe, warithi, wanufaishwa, wawakilishi binafsi wangu/wetu na ni/tuliowateua. Nina/Tuna haki ya kubadilisha au kuondoa Mamlaka haya Kidogo ya Uwakilishi wakati wowote ilivyosemwa; hapa, hata hivyo, taasisi au mhusika yeyote anayeshirikiana na ajenti wangu/wetu wanaweza kutegemea Mamlaka haya Kidogo ya Uwakilishi hadi wapokee nakala yangu/yetu ya uondoaji mamlaka.

Nakala yoyote ambayo imetolewa ya hati hii asilia (hati ya kwanza) itachukuliwa kuwa nakala mwenza asilia ya Mamlaka haya Kidogo ya Uwakilishi. Mamlaka haya Kidogo ya Uwakilishi hayataathiriwa na kushindwa kufanya kitu kisheria katika maisha yangu/yetu, isipokuwa ilivyoahiriwa na sheria.

Mamlaka haya Kidogo ya Uwakilishi yatabakia kutumika kuanzia tarehe ambayo saini imetiwa na kuisha wakati ambapo mamlaka haya
yameondolewa kwa maandishi au tarehe ______________________________, yoyote itakayotangulia.

Imetiwa tarehe ya: ________________________________

Saini: ________________________________________________ ________________________________________

JIMBO LA OHIO )

KAUNTI YA ____________________________ )

Siku hii ____________ ya __________________, 20___, mbele yangu, Mthibitishaji Rasmi katika na kwa ajili ya Kaunti na Jimbo lililotajwa, walikuja wao wenyewe __________________________________________________ na kuthibitisha kutiwa saini kwa hati rasmi iliyopo, na kwamba haya yamefanyika kwa hiari yake/yao.

KWA KUSHUHUDIA HAPA, nimeweka jina langu hapa na kuweka muhuri wangu wa uthibitishaji katika siku na mwaka ulioandikwa hapa juu kwanza.

______________________________________________ Ruhusa Yangu Inaisha: _______________________

Mthibitishaji Rasmi

(MUHURI)

# NUMBER MUHIMU ZA SIMU & TAARIFA MUHIMU

## KUKITOKEA TUKIO LA DHARURA, PIGA NAMBARI 911

**Polisi:**

**Moto:**

**Ubalozi Mdogo:**

## WANAFAMILIA/WATU MUHIMU WA KUWASILIANA NAO MAREKANI

**Jina:**

Simu:

Simu ya Mkononi:

Simu ya Kazini:

Uhusiano:

**Jina:**

Simu:

Simu ya Mkononi:

Simu ya Kazini:

Uhusiano:

## WANAFAMILIA/WATU MUHIMU WA KUWASILIANA NAO KATIKA NCHI YA NYUMBANI

**Jina:**

Simu:

Simu ya Mkononi:

Simu ya Kazini:

Uhusiano:

**Jina:**

Simu:

Simu ya Mkononi:

Kazi:

Uhusiano:

## TAARIFA YA BIMA

**Bima ya Afya**

Kampuni:

Simu:

Nambari ya bima:

**Bima ya Gari**

Kampuni:

Simu:

Nambari ya Bima:

Gari la 1:

Nambari ya VIN/Usajili:

Gari la 2:

Nambari ya VIN/Usajili:

**Bima ya Nyumba**

Kampuni:

Simu:

Nambari ya Bima:

## TAARIFA YA MATIBABU

**Daktari:**

Simu:

**Daktari wa Meno:**

Simu:

**Daktari wa Watoto:**

Simu:

**Hospitali:**

Simu:

**Duka la Dawa:**

Simu:

# REKODI MUHIMU ZA FAMILIA

**Tumia fomu hii kuwekea taarifa zote muhimu ili ziwe pahali pamoja. Weka hati asilia pahali salama (k.m. kwenye kisanduku kilichofungwa).**

## NAMBARI ZA KAZI

**Mwajiri wa 1**

Jina:

Simu:

Msimamizi:

Tarehe ya Kuanza:

Mwakilishi wa Muungano:

Simu:

**Mwajiri wa 2**

Jina:

Simu:

Msimamizi:

Tarehe ya Kuanza:

Mwakilishi wa Muungano:

Simu:

## TAARIFA KUHUSU MAGARI YAKO

**Gari la 1 Aina:**

Nambari ya Gari ya Usajili:

Nambari ya VIN/Kitambulishi:

Mkopo wa Gari:

Bima:

**Gari la 2 Aina:**

Nambari ya Gari ya Usajili:

Nambari ya VIN/Kitambulishi:

Mkopo wa Gari:

Bima:

*Ambatisha nakala ya usajili gari na bima na picha ya kila gari.*

## NAMBARI ZA SHULE/ENEO LA KUTUNZA WATOTO

**Shule ya 1**

Jina la Shule:

Nambari ya Kitambulisho cha Shule

Simu:

Jina la Mtoto:

Jina la Mwalimu:

Jina la Mtoto:

Jina la Mwalimu:

**Shule ya 2**

Jina la Shule:

Nambari ya Kitambulisho cha Shule

Simu:

Jina la Mtoto:

Jina la Mwalimu:

Jina la Mtoto:

Jina la Mwalimu:

## Nambari ya Usalama wa Kijamii/ITIN

Jina:

Nambari:

Jina:

Nambari:

Jina:

Nambari:

Jina:

Nambari:

*Ambatisha nakala ya kila kadi ya usalama wa kijamii.*

# TAARIFA ZA FAMILIA ZA MATIBABU & UTAMBULISHO

**Ambatisha nakala ya cheti cha kuzaliwa, rekodi ya chanjo, na picha za kila mwanafamilia.**

## MWANAFAMILIA WA 1

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa: Mtoaji Kiungo cha Mwili: Ndiyo La

Mizio:

Dawa:

Hali za Kimatibabu & Historia ya Matibabu:

## MWANAFAMILIA WA 2

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa: Mtoaji Kiungo cha Mwili: Ndiyo La

Mizio:

Dawa:

Hali za Kimatibabu & Historia ya Matibabu:

## MWANAFAMILIA WA 3

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa: Mtoaji Kiungo cha Mwili: Ndiyo La

Mizio:

Dawa:

Hali za Kimatibabu & Historia ya Matibabu:

## MWANAFAMILIA WA 4

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa: Mtoaji Kiungo cha Mwili: Ndiyo La

Mizio:

Dawa:

Hali za Kimatibabu & Historia ya Matibabu:

## MWANAFAMILIA WA 5

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa: Mtoaji Kiungo cha Mwili: Ndiyo La

Mizio:

Dawa:

Hali za Kimatibabu & Historia ya Matibabu:

## MWANAFAMILIA WA 6

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa: Mtoaji Kiungo cha Mwili: Ndiyo La

Mizio:

Dawa:

Hali za Kimatibabu & Historia ya Matibabu:

## MWANAFAMILIA WA 7

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa: Mtoaji Kiungo cha Mwili: Ndiyo La

Mizio:

Dawa:

Hali za Kimatibabu & Historia ya Matibabu:

## WATU AMBAO WANAWEZA KUWACHUKUA WATOTO WANGU KUTOKA SHULENI/ENEO LA KUTUNZA WATOTO

| | |
|---|---|
| Jina: | Jina: |
| Tarehe ya Kuzaliwa: | Tarehe ya Kuzaliwa: |
| Simu ya Nyumbani: | Simu ya Nyumbani: |
| Simu ya Mkononi: | Simu ya Mkononi: |
| Uhusiano: | Uhusiano: |

## WATU AMBAO HAWAWEZI KUWACHUKUA WATOTO WANGU KUTOKA SHULENI/ENEO LA KUTUNZA WATOTO

Jina:

Jina:

Jina:

**Tafadhali wajulishe wafanyakazi walioko katika shule ya watoto wako kwamba watu walioandikwa katika sehemu hizi wana ruhusa ya kuwachukua watoto wako au hawana ruhusa. ***Ikiwa kuna amri ya kumzuia mtu, ambatisha nakala ya amri hiyo na uweke nakala nyingine kwenye faili ya shule na/au eneo la kutunza watoto wako.**

# WATU WA KUWASILIANA NAO UKIWA NA SHIDA ZA KISHERIA, WIZI WA UTAMBULISHO UKITOKEA & UDANGANYIFU

**Kwa ajili ya usalama USIANDIKE nambari za kadi zako za mkopo au Nambari za akaunti kwenye hati hii.**

## MAKAMPUNI YA KADI YA MKOPO

**Kadi ya 1**

Kampuni:

Nambari ya Simu Bila Malipo:

Majina yaliyoko kwenye Kadi:

**Kadi ya 2**

Kampuni:

Nambari ya Simu Bila Malipo:

Majina yaliyoko kwenye Kadi:

**Kadi ya 3**

Kampuni:

Nambari ya Simu Bila Malipo:

Majina yaliyoko kwenye Kadi:

**Ripoti wizi wa kadi za mkopo HARAKA!**

## USAIDIZI WA KISHERIA WA KIRAIA

Usaidizi wa Kisheria:

Wakili wa Uhamiaji:

Wakili Mwingine:

## WATU WA KUWASILIANA NAO WAKATI WA MASUALA YA KIFEDHA

**Akaunti ya 1 ya Kutoa Pesa Wakati Wowote**

Benki:

Nambari ya Simu Bila Malipo:

Wanaoweza Kufikia:

**Akaunti ya 2 ya Kutoa Pesa Wakati Wowote**

Benki:

Nambari ya Simu Bila Malipo:

Wanaoweza Kufikia:

**Akaunti ya 1 ya Kuhifadhi Pesa**

Benki:

Nambari ya Simu Bila Malipo:

Wanaoweza Kufikia:

**Akaunti ya 2 ya Kuhifadhi Pesa**

Benki:

Nambari ya Simu Bila Malipo:

Wanaoweza Kufikia:

## WAASILIANI WA MASHIRIKA YA UMMA

Usaidizi kwa Sababu za Vita/Dhuluma za Nyumbani

Kiongozi wa Mashtaka wa Umma:

Ripoti Unyanyasaji wa Mtoto:

# HUDUMA YA DHARURA KWA WANYAMA VIPENZI

## MNYAMA-KIPENZI WA 1

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa:

Aina:

Maelezo mafupi:

Nambari ya Usajili:

Dawa:

Shida za Kimatibabu:

## MNYAMA-KIPENZI WA 2

Jina:

Tarehe ya Kuzaliwa:

Aina:

Maelezo Mafupi:

Nambari ya Usajili:

Dawa:

Shida za Kimatibabu:

## DAKTARI WA WANYAMA

Jina:

Simu:

Anwani:

Simu ya Wakati wa Dharura:

## MAKAZI YA DHARURA KWA AJILI YA WANYAMA VIPENZI

Jina:

Simu:

Anwani:

*Ambatisha picha ya kila mnyama-kipenzi.*

# KIAMBATISHO CHA C:
## NAMBARI MUHIMU

# TAARIFA KWA WAHAMIAJI WALIOZUILIWA & MAWAKILI WA WAHAMIAJI KATIKA OHIO

## MFUMO WA ICE WA MTANDAONI WA KUMPATA ANAYEZUILIWA

**https://locator.ice.gov/odls/homePage.do**

Tumia ukurasa huu kumpata mtu aliye kizuizini anayezuiliwa na ICE, au aliyeachiliwa na ICE kwa sababu yoyote ile ndani ya siku 60 zilizopita. Lazima uandike “Nambari ya mgeni” ya mtu huyo (inayojulikana pia kama “Nambari”) na nchi alipozaliwa. Ikiwa hujui nambari ya mgeni (Nambari) ya mtu huyu, pia unaweza kutafuta kwa kutumia jina lake la kwanza na la ukoo, nchi alipozaliwa, na tarehe ya kuzaliwa. Ukitafuta kwa kutumia jina utapata majina kamili kwenye mfumo, kwa hivyo itakubidi uandike jina la mtu huyo kwa njia kadhaa ama vitofauti tofauti (kwa mfano kwa kutumia kistari ungio, kwa kuandika jina moja pekee la ukoo, n.k.)

KUMBUKA: Mfumo wa Mtandaoni wa Kumpata Anayezuiliwa hauwezi kutafuta rekodi za watu walio chini ya miaka 18.

## OFISI ZA SERIKALI:

### Utekelezaji wa Uhamiaji na Forodha (ICE)

**Cleveland**

925 Keynote Circle
Brooklyn Heights, OH 44131

(216) 749-9200

**Columbus**

50 West Broad St., Ste. 306
Columbus, OH 43215

Anwani Mpya kuanzia tarehe 13 Mei, 2017:
395 East Broad St., Ste. 100
Columbus, OH 43215

### Huduma za Marekani za Uraia na Uhamiaji (USCIS):

**Nambari ya Kitaifa ya Huduma kwa Mteja ya USCIS:** 1 (800) 375-5283

**Ofisi ya Eneo la Cincinnati**
550 Main Street, Room 4001
Cincinnati, OH 45202

**Ofisi ya Eneo la Cleveland**
1240 East 9th Street, Room 501
Cleveland, OH 44199

**Ofisi ya Eneo la Columbus**

50 West Broad St., Ste. 306
Columbus, OH 43215

Anwani Mpya kuanzia tarehe 13 Mei, 2017:
395 East Broad St., Ste. 100
Columbus, OH 43215

## Ofisi Kuu ya Kuchunguza Uhamiaji (EOIR):

**Mahakama ya Uhamiaji ya Cleveland**
801 W. Superior Ave, Suite 13 - 100
Cleveland, OH 44113

(216) 802-1100

**Nambari ya Dharura ya Taarifa ya Kesi**
Taarifa kuhusu hali ya kesi ya watu ambao kesi zao za kuondolewa nchini zinasikizwa mahakamani zipo 24/7. Nambari ya mgeni (A#) inahitajika ili upate taarifa hizi, hata hivyo, mtu yeyote anaweza kupiga simu.

1 (800) 898-7180

## Ulinzi wa Mipaka na Forodha ya Marekani (CBP):

**Sandusky Bay Station**
709 SE Catawba Rd.
Port Clinton, OH 43452

(419) 732-4400

**Erie Station**
7851 Traut Drive
Fairview, PA 16415

(814) 474-4700

## VITUO VYA KUZUILIA WATU:

## Mfumo wa Mtandaoni wa Kupata Kituo cha Uzuiliwaji:

**https://www.ice.gov/detention-facilities**

## Taarifa ya Kiujumla

Wanaozuiliwa hawawezi kupokea simu zinazoingia. Ikiwa unahitaji kuwasiliana na anayezuiliwa ili umwachie ujumbe muhimu, lazima upige simu kupitia nambari ya jengo hilo na upeane majina kamili ya anayezuiliwa, nambari ya usajili ya mgeni, na jina lako na nambari yako ya simu ambayo unaweza kupatikana nayo. Anayezuiliwa atapewa ujumbe wako.

**Kuwatembelea Wanaozuiliwa:** Ili kuwepo na muda wa kutosha wa kuwapitisha wageni kwenye mfumo wa usalama, wageni wote lazima wafike dakika 45 kabla ya wakati uliopangwa ziara hiyo. Wageni lazima waonyeshe kitambulisho halali kilichopeanwa na serikali ya Marekani kinachoweza kuthibitishwa ili waingie kwenye jengo hilo. Watoto wanaotembelea/wanaozuru jengo/eneo hilo lazima waandamane na mlezi aliye mtu mzima (mwenye miaka 18 au zaidi). Watoto hawafai kuwachwa pekee yao kwenye chumba cha kungojea, chumba cha ziara au eneo lingine lolote.

**Kutuma pesa:** Wasiliana na jengo/eneo la uzuiliwaji ili wakupatie taratibu kuhusu jinsi ya kutuma pesa. Wanaozuiliwa wakipokea fedha kupitia barua, watapelekwa kwenye eneo la uchakataji ili pesa hizo ziwekwe kwenye akaunti yao. Ofisa wa uchakataji atapeana risiti za pesa zote zilizopokelewa. Usitume pesa taslimu kupitia barua.

## Jinsi ya Kupeana Dhamana ya Uhamiaji

Dhamana hizi hupeanwa wakati mtu kesi yake inafaa kusikizwa nchini Marekani. Mtu anayepeana pesa za dhamana lazima aonyeshe kitambulisho na kwamba hali yake ya uhamiaji ni halali. Mtu huyu (mwenye jukumu) ako na jukumu la kuhakikisha kwamba mgeni anafika mbele ya ofisa au ajenti wa shirika hili wakati ambapo ameombwa afike hapo. Kwa taarifa kuhusu dhamana, tafadhali piga nambari ya simu ya taarifa ya dhamana ya jengo la uzuiliwaji na omba uzungumze na Ofisa wa Kufukuza Watu anayeshughulikia kesi hiyo. Lazima uwe na jina la ukoo la anayezuiliwa na nambari ya mhamiaji ya usajili kabla ya kupiga simu.

Ili upeane dhamana ya uhamiaji ya mgeni/mhamiaji anayezuiliwa na ICE, lazima upeane dhamana hiyo katika Ofisi ya ERO/ICE ya Cleveland au Columbus (inategemea na eneo linalohusika), Jumatatu hadi Ijumaa (isipokuwa likizo za umma) kati ya saa 9 asubuhi na saa 3 mchana. Njia zinazokubaliwa kulipia dhamana ni kupitia hawala yaani money order, hundi iliyothibishwa au hundi ya keshia. Hii lazima ilipwe kwa “Idara ya Usalama wa Ndani ya Marekani.”

Ikiwa una maswali ya ziada kuhusu dhamana, tafadhali wasiliana na Kituo cha Kusimamia Madeni:

**Kituo cha Kusimamia Madeni**
Kwa: Kitengo cha Dhamana
Sanduku La Posta 5000; Williston, VT 05495-5000: Nambari ya
Simu: (802) 288-(802) 288-7600 | Faksi: (802) 288-1226

## Orodha ya Vituo vyote vya ICE/ERO vinavyokubali Dhamana nchini Marekani:

**https://www.ice.gov/ice-ero-bond-acceptance-facilities**

# VITUO VYA KUZUILIWA KATIKA JIMBO LA OHIO:

## Jela ya Bedford Height City

5661 Perkins Rd.; Bedford Heights, OH 44146

**(440) 786-3254**

Maegesho: Maegesho ya kituo yako karibu na jengo.

Shughuli za Kutekeleza na Kuondoa Nchini (ERO/ICE):
Ofisi ya Kazi za Nje: (216) 535-0510

Taarifa ya dhamana: (216) 535-0510

Kuwatembelea Waliozuiliwa:

Matembezi huwa yanapangwa kutokana na ombi la mtu binafsi pekee. Waliozuiliwa ni sharti wapange ziara siku ya Jumapili na wanakubaliwa kutembelewa mara moja tu kwa wiki kwa dakika 30 pekee, ziara zenyewe zikifaa kuwepo Jumatano, Jumamosi au Juma pili.

Ziara zitadumu kwa dakika 30 pekee. Ikiwa mgeni amesafiri zaidi ya maili 25, ziara zitadumu kwa dakika 90 pekee.

## Kituo cha Usalama cha Kaunti ya Geauga

12450 Merritt Rd.; Chardon, OH 44024

**(440) 279-2009**

Maegesho: Maegesho yako mbele ya jengo.

Shughuli za Kutekeleza na Kuondoa Nchini (ERO/ICE):
Ofisi ya Kazi za Nje: (313) 568-6049

Taarifa ya dhamana: (216) 535-0372

Kuwatembelea Wanaozuiliwa:

Saa zitabandikwa katika kila jumba na kwenye ukumbu wa mapokezi. Saa hizo pia ziko kwenye tovuti ya Idara ya Polisi ya Kaunti ya Geauga.

Wanaozuiliwa wanakubaliwa kutembelewa kwa dakika 60 kwa wiki na wanaweza kuongezewa dakika 30.

## Butler County Correctional Complex

705 Hanover St.; Hamilton, OH 45011

**(513) 785-1191**

Maegesho: Maegesho ya wageni yako mbele ya jengo. Geuka kushoto baada ya kuingia katika eneo la kuegeshea.

Shughuli za Kutekeleza na Kuondoa Nchini (ERO/ICE): Nambari ya Msingi ya Simu ya Ofisi ya Kazi za Nje: (313) 568-6049

Taarifa ya dhamana: (614) 469-2900

Kuwatembelea Wanaozuiliwa:

JINA LA UKOO LA ANAYEZUILIWA LINAANZA NA A - J Jumamosi: Saa 3:00–5:00 asubuhi, Saa 7:00–11:00 jioni, Saa 1:00–3:00 usiku Jumatano: Saa 7:00–11:00 jioni na Saa 1:00–3:00 usiku

JINA LA UKOO LA ANAYEZUILIWA LINAANZA NA K - Z Jumapili: Saa 3:00–5:00 asubuhi, Saa 7:00–11:00 jioni, Saa 1:00–3:00 usiku Alhamisi: Saa 7:00–11:00 jioni na Saa 1:00–3:00 usiku

## Morrow County Correctional Facility

101 Home Rd.; Mt. Gilead, OH 43338

**(419) 947-4845**

Kuegesha: Pahali pa kuegeshea katika kituo pako karibu na jengo.

Shughuli za Kutekeleza na Kuondoa Nchini (ERO/ICE):
Ofisi ya Kazi za Nje: (313) 568-6049

Taarifa ya Dhamana: (614) 469-2900

Kuwatembelea Wanaozuiliwa:

Wanaozuiliwa wa Kiume:
Jumamosi: Saa 7:00–9:00 mchana na Saa 1:00–3:00 usiku

Wanaozuiliwa wa Kike:
Jumapili: Saa 7:00–9:00 mchana na Saa 1:00–3:00 usiku

## Northeast Ohio Correctional Center

2240 Hubbard Rd.; Youngstown, OH 44505
**(330) 746-3777**

Maegesho: Maegesho ya wageni yako kushoto mwa njia na pamewekewa alama.

Kuwatembelea Wanaozuiliwa:

Wageni wanaruhusiwa kuwa watu sita (6) pekee walioidhinishwa kwa wakati moja. Wageni sharti waidhinishwe kabla ya ziara. Tuma barua pepe kwa**neohiovisit@corecivic.com**, kabla ya siku ya Jumapili kabla ya wiki ambayo unafaa kumtembelea anayezuiliwa.

Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi: Saa 3:30-5:30 jioni

Ziara zinapaswa kudumu kwa saa moja (1) pekee.

## Seneca County Jail

3040 South State Rte. 100; Tiffin, OH 44883
**(419) 448-5074**

Maegesho:: Maegesho yako mbele ya jengo.

Shughuli za Kutekeleza na Kuondoa Nchini (ERO/ICE):
Ofisi ya Kazi za Nje: (313) 568-6049

Taarifa ya dhamana: (216) 535-0372

Kuwatembelea Wanaozuiliwa:

Jumapili:
Wanaume: Saa 2:00–4:00 asubuhi, Saa 6:30–10:00 jioni, Saa 11:30-1:30 usiku Wanawake: Saa 4:00-5:00 asubuhi, Saa 1:30-2:30 usiku

## Ubalozi wa Somalia

Embassy in Washington, D.C.
Address: 1705 Desales St NW, Washington, DC 20036
Hours: Open · Closes 5PM
Phone: (202) 296-0570

## Ubalozi wa Uhabeshi

3506 International Dr NW, Washington, DC 20008
Hours: Open · Closes 5PM
Phone: (202) 364-1200
Ambassador: Girma Birru

## Ubalozi Mdogo wa Uhabeshi Jijini New York, Marekani

866 2nd Avenue, 3rd Floor
New York, NY 10017
United States
Telephone(+1) (212) 421-1830
Fax(+1) (646) 756-4690
EMAILethiopia@un.int

## Mkuu wa Ubalozi Mdogo wa Uhabeshi Jijini Chicago, Marekani

5041 N. Kenmore Avenue
Chicago, IL 60640
United States
Tel (+1) (773) 681-4925

## Ubalozi wa Kenya

Address: 2249 R St NW, Washington, DC 20008
Hours: Closes soon: 4PM · Opens 9AM Fri
Phone: (202) 387-6101

Afrika Kusini Jamhuri ya Afrika Kusini
Taarifa ya Mawasiliano ya Ofisi ya Balozi Mdogo wa Kigeni

consular.wa@dirco.gov.za
Washington, DC (202) 274-7992 (202) 244-9417
Chicago, IL (312) 939-7929 (312) 939-2588
Los Angeles, CA (323) 651-0902 (323) 651-5969
New York, NY (212) 213-4880 (212) 213-0102

## Ubalozi Mdogo wa Kenya jijini New York

866 UN Plaza Suite 302
New York, NY 10017 U.S.A.
Tel: (212) 421 4741
Fax: (212) 486 1985

## Ubalozi wa Jamhuri ya Sudani

2210 Massachusetts Ave
Washington DC,20008
Phone: 202-338-8565
Fax: 202-667-2406
Hours of Operation Monday - Friday 9a.m to 5p.m

## Ubalozi wa Jamhuri ya Jibuti

1156 15th Street NW Suite 515
Washington, DC 20005 USA
(202) 331-0270

Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

Advocates for Basic Legal Equality, Inc. (ABLE) ni kampuni ya kisheria ya eneo kubwa isiyo ya kifaida ambayo inatoa usaidizi wa kisheria wa kiraia wa hali ya juu ili kusaidia vikundi na watu binafsi ambao wako na mapato ya chini na wanaostahiki walioko magharibi mwa Ohio ili waweze kujitegemea, na kupata nafasi sawa za haki na kiuchumi.

**immigration.ablelaw.org**
**ablelaw.org**

**/ABLELawInc**

**linkedin.ablelaw.org**

Omba usaidizi wa kisheria wa bila malipo kwenye mtandao kupitia Legal Aid Line:

**LegalAidLine.org**


130 W. Second St., Ste. 700 East
Dayton, OH 45402

(937) 228-8104 | (800) 837-0814

FAKSI: (937) 535-4600
TTY: (888) 545-9497

525 Jefferson Ave., Ste. 300
Toledo, OH 43604

(419) 255-0814 | (800) 837-0814

FAKSI: (419) 259-2880
TTY: (888) 545-9497